# CLASS 5 KISWAHILI END TERM 1 2020

***Soma kifungu hiki kisha ujaze pengo kwa neno linalofaa zaidi.***

Nguo ____1____ zilijaa vumbi ____2_____. Alikuwa ameangushwa na mwenzake ____3____ uwanjani. Mguu ____4_____ wa kushoto ulikuwa umeumia. ____5____ mwingine haukuwa umeumia hata kidogo. Aliinuka na wenzake wakaanza ____6____. Jambo hilo lilimfanya aanze _____7_____ kwikwikwi. Rafiki _____8_____ wa dhati alimwonea huruma na kumwomba _____9____. Wote walikumbatiana na kuelekea ____10____. Waliketi madawatini ____11____ na kutulia tuli. Mwalimu ____12_____ aliwakuta wakisoma somo la Hisababti. Alifurahishwa na bidii ______13____ za mchwa. Aliwaahidi kuwanunulia zawadi na ____14____ siku ya kufunga. Waliingoja siku hiyo kwa hamu na ____15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. zake | B. yake | C. wake | D. chake |
| 2. | A. kingi | B. mengi | C. mingi | D. jingi |
| 3. | A. wakikimbiliwa | B. akikimbizana | C. wakikimbizana | D. akiketi |
| 4. | A. yake | B. wake | C. lake | D. zake |
| 5. | A. Hiyo | B. Huyo | C. Hio | D. Huo |
| 6. | A. kumcheka | B. kumlilia | C. kumchekelewa | D. kumhuzunisha |
| 7. | A. kucheka | B. kununa | C. kulia | D. kukasirika |
| 8. | A. wake | B. yake | C. zake | D. lake |
| 9. | A. ruhusa | B. idhini | C. ombi | D. msamaha |
| 10. | A. darasani | B. maabadini | C. ugani | D. bustanini |
| 11. | A. yao | B. mwao | C. pao | D. vyao |
| 12. | A. aliyetoka | B. anayeingia | C. atakaloingia | D. alipoingia |
| 13. | A. wao | B. zao | C. yao | D. chao |
| 14. | A. kuwapa | B. kuwapea | C. kuwanyima | D. kuwarudi |
| 15. | A. gamu | B. ulimbo | C. zamu | D. shauku |



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Kutoka swali la 16 - 30, jibu swali kulingana na maagizo uliyopewa***

**16.** Chagua sentensi sahihi
A. Wavulana warefu wawili.
B. Wavulana wawili warefu.
C. Wasichana warembo wawili.
D. Wasichana warefu watatu.

**17.** Ni nini maana ya msemo: *chafua moyo*?
A. Kufurahia
B. Kutamauka
C. Kuwa mchafu
D. Kukasirisha

**18.** Kanusha: *Alimtukana na kumkemea.*
A. Hakumtukana wala kumkemea.
B. Hakumtukana na kumkemea.
C. Hakumtukana lakini alimkemea.
D. Hakumtukana alimkemea.

**19.** Subui kwa tarakimu ni
A. $\frac{1}{3}$ B. $\frac{1}{8}$
C. $\frac{1}{7}$ D. $\frac{1}{5}$

**20.** Jipu na kidonda hutoa usaha lakini jeraha hutoa
A. ute B. damu
C. maji D. matongo

**21.** Tunasema baridi kama
A. yabisi B. chuma
C. umande D. barafu

**22.** Mtoto wa ndugu yako wa kike utamwitaje?
A. Mpwa B. Dada
C. Mama D. Binamu

**23.** Jaza pengo kwa kiulizi mwafaka.
*Unataka nguo yako ishonwe________?*
A. aje B. kipi
C. gani D. vipi

**24.** Kamilisha sentensi:
*Kabati __________ huwa sokoni.*
A. cheupe B. jeupe
C. nyeusi D. lekundu

**25.** Mwanafunzi aliandika hadithi kwa hivyo hadithi ______
A. iliandikika
B. iliandikiwa
C. iliandikwa
D. iliandaliwa

**26.** Nomino **mikoba** ni katika ngeli gani?
A. I-I B. U-I
C. YA - YA D. LI - YA

**27.** Je, kikembe cha ndege huitwaje?
A. Kinda B. Nyuni
C. Kifaranga D. Jana

**28.** Mtu ambaye hujenga nyumba kwa mawe ni
A. seremala B. fundi
C. mwashi D. mhunzi

**29.** Ni nini kinyume cha neno **simama**?
A. Lala B. Kaa
C. Usisimame D. Inuka

**30.** Udogo wa neno **mto** ni
A. kimto B. kito
C. kijijito D. kijito

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.***

Ilikuwa siku ya Jumamosi alfajiri wakati wa likizo ya Aprili. Tulia, Nyungu, Mweke na Chuma waliondoka kwenda mawindoni. Walikuwa wamefuatana kama mtu na kivuli chake na mbwa wao sita. Guru ndiye aliyekuwa mbwa stadi wa kuwinda.

Baada ya kutembea kwa muda mrefu, wavulana hawa walifika kwenye mti mkubwa. Kando ya mti huo, palikuwa na kichaka kikubwa chenye miti mingi na nyasi ndefu.

Punde si punde, swara wawili walijitokeza, wakitimua mbio. Kila mmoja alishika njia yake. Guru na wenzake walianza mbio zao kuwafuata wanyama wale.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

"Huyo! Huyo!" Alipaza sauti Chuma ambaye alionekana kuwa alikuwa amewazidi umri lakini si kwa kimo.

Mbwa watatu walimfuata swara mmoja na wengine yule swara mwingine. Tulia na Nyungu walimfuata Guru. Mweke na Chuma nao walimfuata swara yule mwingine.

Baada ya kuvuka mto, Guru na wenzake wawili walishika windo lao. Alikuwa swara mnene. Mweke na Chuma alijiunga na wenzao. Swara yule mwingine alikuwa amejiokoa na kwenda zake.

Vijana hawa wanne walimchinja swara yule. Walikoka moto na kuanza kuchoma nyama. Harufu nzuri ilijaa hewani. Mate yalianza kuwadondoka. Chuma alianza kuwakatia wengine nyama.

Ghafla bin vuu walisikia sauti ya askaripori. "Mikono juu". Walitetemeka kwa woga. Wote walitiwa mbaroni na kutiwa pingu. Wazazi na wazee wa kijiji waliitwa mara moja. Vijana wale walilia sana. Baada ya kuomba msamaha, walisamehewa.

Walipofika shuleni walianza chama cha kutunza miti na pia wanyama. Adhabu yao ikawa kutunza miti pale kijijini.

**31.** Wawindaji hawa walikuwa wangapi?
A. Sita
B. Watatu
C. Watano
D. Wanne

**32.** Nani alikuwa stadi sana wa kuwinda?
A. Mbwa mmoja
B. Mbwa wote
C. Mvuli mmoja
D. Watu wote

**33.** Ni kweli kusema kuwa
A. waliwaona askari kabla ya kuingia msituni.
B. hawakuona mto wowote.
C. walifika kichakani baada ya muda mrefu.
D. wawindaji wale walikuwa waoga.

**34.** Wawindaji haramu wanafaa kuitwa
A. wasasi
B. majangili
C. wakora
D. magaidi

**35.** Ni nini maana ya msemo **shika njia**?
A. Kwenda mbio
B. Kuanguka chini
C. Kuteleza mchangani
D. Kwenda zako

**36.** Ni kijana yupi alikuwa mzee zaidi ya wengine?
A. Mweke
B. Chuma
C. Tulia
D. Nyungu

**37.** Swara aliyeshikwa alifukuzwa na mbwa wangapi?
A. Wanne
B. Sita
C. Watatu
D. Wawili

**38.** Kudondokwa na mate ni ishara ya
A. wivu
B. tamaa
C. shibe
D. njaa

**39.** Unafikiri ni kwa nini wawindaji hawakumla swara mzima?
A. Swara alitoroka
B. Wote walishiba
C. Waliwapa mbwa
D. Walishikwa na polisi

**40.** Adhabu waliopewa wanafunzi wale ilikuwa ipi?
A. Kuchunga mimea kijijini.
B. Kutunza miti pale shuleni.
C. Kutunza wanyama kijini.
D. Kuanza chama cha wanyama.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50***

Kwa mara nyingine, maelfu ya watu nchini Kenya wamekumbwa na upungufu wa chakula. Janga la njaa limewakodolea macho na watu wengi kwa sasa wanalala njaa. Nchi yetu imekuwa ikikumbwa na matatizo kama mafuriko, ufisadi,uhalifu na hata ugaidi.

Viongozi wetu ndio chanzo cha matatizo mengi kwani hawatujali. Kiongozi achanguliwapo, huendelea kujitafutia mali zaidi na kusahahu maskini ambao walikosa usingizi na kumchagua. Shida zinaongezeka kila siku kwa sababu ya viongozi hawa.

Kuna mikakati mingi ambayo serikali huiweka. Jambo la kukatisha tamaa ni kuwa mikakati yenyewe haitekelezwi. Kwani umesahau nzige ambao walituvamia juzi? Waziri ambaye alipigwa kalamu alishindwa kusaidia wakulima. Nao wakaendelea kuhesabu hasara ya wadudu hao.

Mipango mizuri ndiyo inahitajika katika kila jambo. Viongozi waache kuwa na tamaa ya fisi. Hakuna jambo au tatizo ambalo haliwezi kusuluhishwa hapa nchini. Suala la njaa litasuluhishwa ikiwa serikali itawasaidia wakulima. Bei ya mbegu, mbolea na kemikali isiwe ya juu.

Hata kama wanafunzi wa shule za msingi hawachagui viongozi wa nchi, wao huchagua viongozi wa shuleni. Hivyo basi kila mmoja ana haki ya kujieleza ikiwa viongozi hawafanyi kazi. Ikiwa kazi yao ni kuketi tu, hawana budi kurudi nyumbani na kuchaguliwe wengine.

Ikiwa wewe ni kiongozi, ni lazima uwahudumie wale waliokuchagua.

**41.** Jambo ambalo linawatatiza wananchi ni
A. wizi
B. janga
C. shibe
D. njaa

**42.** Lipi si tatizo linalotatiza wananchi wa Kenya?
A. Ukame
B. Ugaidi
C. Uhalifu
D. Kutoa hongo

**43.** Ni nini husababisha shida katika nchi yetu?
A. Wananchi
B. Wadudu
C. Viongozi
D. Mazingira

**44.** Kulingana na kifungu hiki, ni kweli kusema kuwa
A. shida za nchi hazina suluhisho.
B. wananchi hujitolea wakichagua viongozi.
C. viongozi wote ni wabaya.
D. watu wengi huwa wafisadi.

**45.** Maana ya msemo **alipigwa kalamu** ni
A. kuchukuliwa hatua
B. kuadhibiwa vikali
C. kufutwa kazi
D. kuishiwa na maarifa

**46.** Tamaa ya viongozi wetu nchini inafananishwa na
A. wananchi
B. nzige
C. wanyama
D. fisi

**47.** Wakulima watasaidikaje kulingana na kifungu hiki?
A. Bei ya mbolea isiwe juu.
B. Serikali iwape soko nzuri.
C. Kupewa pesa za kulima.
D. Serikali iwape wakulima mbegu.

**48.** Ni kweli kusema kuwa
A. viongozi wa shule hawachaguliwi.
B. wanafunzi hawana haki yoyote.
C. walimu huchagua viongozi shuleni.
D. hata wanafunzi huchaguana.

**49.** Tunafaa kuchaguana tena ikiwa viongozi wetu
A. ni wenye bidii.
B. hawafanyi kazi.
C. ni karimu na wazembe.
D. ni wazuri.

**50.** Kichwa mwafaka cha kifungu hiki ni
A. Shida ya uongozi
B. Wadudu nchini
C. Viongozi shuleni
D. Janga la njaa



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com